**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU**

**TAREHE 15.11.2025**

MAWASILIANO:
1. O766854321 – MKUU WA SHULE
2. 0747025279 – M/MKUU WA SHULE
3. 0766390729 – M/MKUU WA SHULE

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………………………
S.L.P …………………………………………………….
……………………………………………………………….

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU KWA WANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA JANUARI 2026.**

## 1. UTANGULIZI.

- Mwanafunzi tajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2026.. HONGERA SANA
- Shule ya sekondari ya wasichana Simiyu (Simiyu girls secondary school) ni shule ya bweni inayopatikana katika mkoa wa Simiyu ndani ya halmashauri ya wilaya ya Bariadi katika Kijiji cha **IGEGU**. Aidha Shule hii inapatikana umbali wa kilomita 45 kutoka mji wa Bariadi au umbali wa kilomita 25 kutoka mji mdogo wa Lamadi kando kando mwa barabara ya Bariadi - Lamadi
- Namna ya kufika shule ilipo.
  Ukitokea Bariadi tumia usafiri wa basi, nauli ni Tsh. 3000/= na kushukia kituo cha igegu kisha kutumia usafiri wa pikipiki kufika shule. AU waombe wakushushe simiyu girls. Hii itawahusu pia wote wanaotumia barabara hii inayo pita Bariadi kutoka mikoa mingine kama Dar es salaam, Dododma , Tabora na Shinyanga
  Ukitoka Lamadi, tumia usafiri wa basi, nauli ni Tsh 2000/= na kuomba wakushushe simiyu girls au wakushushe kituo cha Igegu. Hii inawahusu pia wanaotoka mikoa ya Mwanza na Mara.
- Muhula wa masomo unatarajiwa kuanza tarehe 13/01/2026. Hivyo mwanafunzi aripoti shule tarehe 13/1/2026 siku ya jumanne. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/01/2026 saa 10.00 jioni.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1. SARE YA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare za shule kama zinavyobainishwa hapa chini.

i. Mashati meupe mawili(2) yenye mikono mifupi yanayoishia kwenye kiwiko.( kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi mashati yao yawe yenye mikono mirefu).

ii. Sketi mbili za drafti mshono linda box kubwa mbele na nyuma na malinda madogo mawili kwa kila upande baada ya linda kubwa.( kitambaa kimeambatishwa). Urefu wa sketi ni sentimita 7 chini ya goti. Kwa wanafunzi wa kiislam na wale wenye ulemavu wa ngozi sketi zao ziwe ndefu kiasi.




*Rangi ya kitambaa cha sketi*




***Mchoro wa mshono wa sketi***

iii. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kisigino kifupi na vinavyofungwa na Kamba jozi mbili (2)
iv. Soksi nyeupe ndefu zinazoishia kwenye magoti(free size stocking) jozi tano(5)
v. Kwa wanafunzi wa kiislam waje na juba nyeupe mbili watakazovaa wakiwa darasani tu.
vi. T shirt 1 ya rangi nyeusi yenye kola na nzito atavaa akiwa darasani tu.
vii. Sweta 1 la rangi ya damu ya mzee (rangi ya maruni) atavaa akiwa darasani tu.
viii. magauni ya kushindia (shamba dress) mawili (2) kitambaa esteem namba 1 rangi ya blue bahari( light blue) mshono wa solo atakayovaa baada ya kutoka darasani. Magauni haya yawe na urefu wa sentimita 7 chini ya goti na yenye mikono mfupi kama mchoro unavyoonyesha. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na juba ya rangi ya blue bahari atakayoivaa pamoja na gauni hili. Kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi magauni yao yawe na mikono mirefu.



Rangi ya kitambaa cha gauni




*Michoro ya mshono wa gauni*


ix. Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo.
x. Soksi nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo
xi. Track suit jozi 1 rangi nyeusi yenye mistari myeupe pembeni kwa ajili ya michezo na wakati wa usiku kuzuia baridi.
xii. Bukta 1 na tisheti 1 nyeusi zenye mistari myeupe pembeni kwa ajili ya michezo

## 2.2. MAHITAJI MENGINE

i. Kadi ya Bima ya afya ya **NHIF.** Kama hana bima basi siku ya kuripoti njoo na pesa kiasi cha Tsh. **50,400** kwa ajili ya kumkatia bima hiyo kwa mwaka mmoja. Hii ni **LAZIMA**.
ii. Ream 2 kwa mwaka (**DOUBLE A**)
iii. Daftari 10 (counter book) kwa ajili ya kazi za darasani
iv. Daftari 10 ndogo kwa ajili ya mazoezi yake binafsi ya kila siku
v. Kalamu za wino na penseli za kutosha
vi. Mathematical set 1
vii. Kamusi ya kiingereza (OXFORD DICTIONARY) 1
viii. Godoro 1 size **$2^1/_2$ *6**
ix. Blanketi 1, shuka 2 (1 rangi ya blue nyingine rangi ya pinki), mto wenye foronya za rangi ya shuka (sio lazima), na chandarua chenye rangi neupe chenye pembe 4.
x. Sanduku la bati la kuhifadhia vitu vyake
xi. Begi la kubebea daftari
xii. Vyombo vya chakula yaani sahani,kikombe,kijiko na chupa ya chai (chupa ya chai si lazima) na chombo chenye ujazo wa lita 5 kwa ajili ya kutunza maji yake ya kunywa.
xiii. Taulo 1, kandambili jozi 1 na kanga jozi 1 kwa matumizi wakati wa kuoga
xiv. Nguo za ndani za kutosha
xv. Rain boot jozi 1 ya rangi nyeusi ataivaa wakati wa mvua
xvi. Sabuni za kuogea,sabuni za kufulia,dawa ya meno, mswaki,kitana na mafuta ya kupaka ngozi yasiyo na harufu kali
xvii. Ndoo ndogo 1 yenye ujazo wa lita 10

## 2.3. VIFAA VYA USAFI

i. Squeezer 1 (kifaa cha kukaushia maji)
ii. Jembe 1 na mpini wake
iii. Fagio la ndani (soft bloom) 1 **AU** fagio la nje (hard bloom) 1
iv. Toilet cleaner (ARO) Lita moja



**TOILET CLEANER**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Tekinolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;

(i) Kutunza mali za shule

**MUHIMU:**

1. Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa **mama, baba, kaka ama dada tu** na **siyo mtu mwingine**. Taarifa za misiba ziletwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule siyo kwa mwanafunzi. Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.

2. Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika Bwalo.

3. Wageni wanao tambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja kwa muhula yaani (mara 2 kwa mwaka)

4. Wakati wa likizo, mwanafunzi atalazimika kwenda nyumbani na si kwingineko.

## 3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/ kupata mimba
9. Kuolewa ama kuwekwa kimada
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu wengine.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kumiliki na kutumia simu ya mkononi shuleni.

## 4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI.

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Form for Medical Examination) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

(iv) Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kwa kikamilifu.

**MWL. HURUMA A. MTINDYA**
**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
SIMIYU GIRLS SEC. SCHOOL
P.O. BOX
BARIADI

**FORM NO. 1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA, PRESIDENTS' OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants. Pupil's full name……………………………………………………………………………

Age/Years…………………………………Sex……………………………………

Blood found (red and White)…………………………………………………………….

Stool examination:……………………………………………………………………….

Urinalysis:………………………………………………………………………………..

Venereal Diseases test:…………………………………………………………………..

T.B. test:…………………………………………………………………………………

Eye Test:…………………………………………………………………………………

Ears:………………………………………………………………………………………

Chest:……………………………………………………………………………………..

Spleen:……………………………………………………………………………………

Abdomen:………………………………………………………………………………..

Urine for Pregnant:………………………………………………………………………

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc.

Infection chronic or family disease etc.

…………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:…………………………………………………………..

Designation:……………………………………………………….
Station:…………………………………..Date:……………………

Official Stamp: ……………………

**FORM NO. 2**

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU

## TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………..
2. KABILA…………………………………………………………………...
3. TAREHE YA KUZALIWA……….MWEZI……………MWAKA…………

4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA………………………………….
5. MKOA WA……………………………………………………………..

6. DINI……………………DHEHEBU…………………………………......
7. JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………
   (Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
8. ANWANI YA MZAZI/MLEZI… .KIJIJI …………………………….
   KATA …………………………
   . TARAFA…………………………….
   WILAYA…………………………… MKOA…………………………….
   Na. ya simu……………………………………………….
9. KAZI YA BABA/MLEZI…………………………………………………….
10. KAZI YA MAMA……………………………………………………………...

11. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).

    …………………………………………………………………………………….
    …………………………………………………………………………………….
    …………………………………………………………………………………….

12. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (mawili tu), anuani zao kamili na Nmba zao za Simu.

(a) Ndugu………………………………………….. Uhusiano……………………
…………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………..

**PICHA**

(b) Ndugu…………………………………………… Uhusiano…………………
…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………….

**PICHA**

TAREHE:………………………...

……………………………………

**SAINI YA MWANAFUNZI**

**FORM NO. 3 MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi………………………………………….                (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Nahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya mwanafunzi……………………………………

Tarehe……………………………………………………

Shahidi

Jina kamili………………………………………………

Saini…………………………………………………….

Tarehe…………………………………………………….

## FORM NO. 4

**A: AHADI YA MZAZI:**

Mimi………………………………………………………… (jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa……………………………….Kidato cha…………………. Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

Saini ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………….

Anuani kamili………………………………………………………………………….

Simu:……………………………………….

Tarehe:……………………………………….